Dominate

NINI UNAFANYA
NA MAISHA YAKO?

Severino I. Lubugo

Dominate

NINI UNAFANYA
NA MAISHA YAKO?

Severino I. Lubugo

NINI UNAFANYA NA MAISHA YAKO?

DOMINATE

SEVERINO I. LUBUGO

Mawasiliano ya Mwandishi

Simu: **0654974887**

Email: lubugo60@gmail.com

Facebook: severino lubugo

Instagram: severino lubugo

Toleo la 1: 2022

ISBN:987-992-40-874-6

Haki zote zimehifadhiwa

Hairuhusiwi kunakiri kitabu hiki bila idhini ya mwandishi

Kimechapishwa na;

DREAM HIGHER Prints

0784256509

Dar es Salaam-Tanzania

YALIYOMO

UTANGULIZI.....5

SURA YA KWANZA.....9

KILA KITU HAKITOSHI.....9

Kundi la 1: KILA KITU HAKITOSHI (Haiwezekani)...12

Kundi la 2: KILA KITU KINAWEZEKANA (Nini naweza kufanya kwa "vichache hivi mkononi mwangu").....16

SURA YA PILI..... **Error! Bookmark not defined.**

MGOGORO WA UTAMBULISHO**Error! Bookmark not defined.**

VITA ILIYOPO NI; Kukubali KUBADILIKA na KUJITOA KWENYE U-KAWAIDA dhibi ya "HOFU" KUWA HAKUNA MAISHA NJE YA U-KAWAIDA. **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA TATU ..... **Error! Bookmark not defined.**

KITU KIKUBWA NJE YA KILE UNACHOHITAJI: KAZI. ..... **Error! Bookmark not defined.**

KAZI ni mkakati wa KUFANYA KITU KIKUBWA KULIKO "kujitafutia mahitaji yako", KAZI ni KUFANYA KUSUDI. ... **Error! Bookmark not defined.**

KIPAJI..... **Error! Bookmark not defined.**

KUSUDI ..... **Error! Bookmark not defined.**

MAONO..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA NNE..... **Error! Bookmark not defined.**

TUNAFANYA BIASHARA: TATUA HILO TATIZO. ... **Error! Bookmark not defined.**

FURSA YA KUTATUA MATATIZO YA WATU. ..... **Error! Bookmark not defined.**

DUNIA IMEJAA UTELE (Utele = Utajiri)..... **Error! Bookmark not defined.**

HUWEZI KUPATA UTAJIRI - MPAKA UONE MATAJIRI ..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA TANO..... **Error! Bookmark not defined.**

ENEO LA KUJIAMINI .... **Error! Bookmark not defined.**

Tatizo gani wewe unaenda kulitatua?..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA SITA ..... **Error! Bookmark not defined.**

CHAGUA UWANJA WAKO**Error! Bookmark not defined.**

Ni ulimwengu wa biashara na kila sehemu kuna fursa, ila sio kila fursa inakuhusu.**Error! Bookmark not defined.**

FANYA MAAMUZI: uwanja/eneo lipi LITAKUPA MATOKEO UNAYOTARAJIA?**Error! Bookmark not defined.**

SURA YA SABA ..... **Error! Bookmark not defined.**

JINSI YA KUANZA ..... **Error! Bookmark not defined.**

#1 kujipanga ..... **Error! Bookmark not defined.**

#2 Angalia fursa ..... **Error! Bookmark not defined.**

#3 LENGA KWENYE MATOKEO: Fanya na Jifunze ..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA NANE..... **Error! Bookmark not defined.**

MAFANIKIO NI KWA WALE WATU “wachache” WALIOTAYARI KUFANYA, KUJIFUNZA, KUFANIKIWA HUKU WAKIWA WANAENDELEA KUFANYA..... **Error! Bookmark not defined.**

SURA YA TISA ..... **Error! Bookmark not defined.**

WITO KWA WAJASILIAMALI**Error! Bookmark not defined.**

UTANGULIZI

Tupo kwenye tatizo na wengi bado hawajui kama tupo kwenye tatizo.

Ukiangalia maisha ya vijana wengi utagundua kuwa WAMEKWAMA MAHALI!

Hawapigi hatua, wala hawaendelei na maisha yao.

Nimekutana na vijana – wahitimu wa vyuo, wasomi, wenye utayari na shauku kubwa ya kufanya kazi. Vijana hawa muda mfupi baada ya kumaliza vyuo ndio walikuja kuelewa kile walichokuwa wanafikiri kipo – HAKIPO.

Ile ndoto nzuri waliyosimuliwa zamani na ndugu na marafiki au na wazazi kwamba baada ya kumaliza masomo ni kazi: kuajiriwa, au kujiajiri, kisha kuwa na hela za kununua gari na kujenga, kuanzisha familia na kufanikiwa, SIO KWELI. Haipo! na haiwezekani.

Kazi, HAKUNA.

Biashara, HAWANA MTAJI.

kuingia kokote kule hata kwa kujitolea tu, HAWANA mtu wa KUWAUNGANISHA ili kuweza kupata kazi kwa haraka.

Maisha yao yako kwenye sitofahamu. Wengi hawajui na hawaelewi tatizo linalowakabili ni nini? linatokana na nini? na linaweza kutatuliwa na nani?

Ukisikiliza mazungumzo yanayoendelea mitaani utaelewa kuwa hili tatizo halina ufumbuzi kwa wengi. Kwa sababu badala ya kuwa na mazungumzo ya kutafuta suluhu – wengi wanalalamika, wanalaumu na kuwaona wengine ndio waliosababisha wao kufika hapo walipo.

Kwa wengi tatizo linatokana na mfumo wa elimu, serikali iliyopo madarakani, mjomba wake kushindwa kumpa mtaji, umaskini wa familia yake, watu kutokuwa na utayari wa kusikiliza mawazo ya wengine na sababu nyingine nyingi kama hizo.

**

Baada ya kuwa mhitimu wa chuo na kupita kwenye sitofahamu kama hiyo, nimekuja kujua UKOSEFU WA AJIRA sio tatizo linaloweza kutatuliwa na serikali wala sio tatizo linaweza kutatuliwa na mabadiliko ya mfumo wa elimu. Sio upatikanaji wa mitaji wala sio kubadilika mitazamo ya wengine wanapokuwa wanasikiliza mawazo na ubunifu

wa wengine. Kila kitu kinachohusisha mabadiliko nje ya mtu ni tofauti kabisa na kile kinachoweza kuleta tofauti.

Swali sahihi la kujiuliza, SIO kazi gani nitafanya inayolipa vizuri? Wala SIO biashara gani itanitajirisha kwa haraka?

Swali sahihi la kujiuliza ni “NINI NITAFANYA NA MAISHA YANGU?”

Ukosefu wa ajira ni janga la ki-dunia kila mahali lipo, kila nchi lipo. Tunatofautiana tu viwango na namna yetu ya kulitazama.

Hakuna serikali yoyote duniani iliyoweza kuwahakikishia wananchi wake wote kupata ajira wala hakuna mtu au mwanasiasa yoyote anaweza kufanya hilo. Ila mtu yoyote anaweza KUBADILI MTAZAMO WAKE kwa kuacha kusubiri wengine kuja kumsaidia ila KUJISAIDIA MWENYEWE – mtu kama huyo anaweza kuleta utofauti na kuweza kutatua tatizo la ukosefu wa ajira.

Kitabu hiki ni kwa ajili ya kutatua tatizo.

Kwa watu wote wanaofikiri namna ya kuleta tofauti, waliofanya maamuzi ya kuleta tofauti, na wanaoendelea kufanya kila

wanachokifanya ili kuleta tofauti. HIKI NI KWA AJILI YAO.

Swali sahihi kijiuliza ni, NINI NAFANYA NA MAISHA YANGU?

SURA YA KWANZA

KILA KITU HAKITOSHI

Tarehe 19/7/2019 majira fulani hivi ya jioni nilikuwa natoka kufanya mtihani wa mwisho (wa degree) kumaliza shahada yangu ya awali. Jioni ile nilikuwa nawaza kuwa sasa “nimemaliza shule”. Ile safari ya takribani miaka 20 ilikuwa tayari imefikia ukingoni, nilikuwa tayari kuingia kwenye ulimwengu wa ajira.

Jioni ile nikiwa mmoja kati ya wahitimu wengi katika viwanja vya T.I.A sikuwa naelewa chochote: wakati wenzangu wanaendelea na shangwe za kumaliza masomo, mimi nilikuwa na maswali yasiyo na mwisho!

Maswali yaliyochosha kichwa changu. Maswali yaliyotosha kunifanya kuona kero kwa kila kilichokuwa kinaendelea; kupiga picha za kumbukumbu, kucheza muziki na kufurahia na marafiki.

Sina uhakika sana kama nilifanya kitu sahihi ila sikuweza kufanya kingine zaidi ya hilo. Kichwani kwangu kulikuwa na swali moja kubwa; BAADA YA HAPA NINI KINAFUATA?

Kesho asubuhi nitakwenda wapi baada ya kuamka? Baada ya kulivua rasmi jina “mwanafunzi” – nitakuwa najitambulisha kama nani tena?

Kwa ujumla nilipoteza sehemu ya kwenda kila siku, nilipoteza marafiki na zaidi nilipoteza u-kawaida wa maisha niliyokuwa nimeyazoea. Ila hayo yote hayakuwa tatizo. Tatizo kubwa lilikuwa “kila kitu hakitoshi.

NDOTO NILIKUWANAYO; Ila SIKUWA NAONA UWEZEKANO WA KUIISHI “SASA”.

Tofauti na wengine, waliokuwa na ndoto za kufanya kazi kwenye taasisi kubwa kama *TRA*, *Benki*, *PSPF* na mashirika mengine mbalimbali. Ndoto yangu kubwa ilikuwa ni kujiajiri.

Nilihusudu sana wazo la ujasiriamali. Kila niliposikia kuhusu ujasiriamali fahamu zangu ziliniambia huo ndio uwanja pekee unaonifaa na nilikuwa tayari kuingia humo.

TATIZO LILILOKUWEPO ni kuwa Sikuona uwezekano wa kuanza kuiishi ndoto hiyo kwa wakati niliokuwa nao.

KWA NANI? kwa sababu KILA KITU HAKITOSHI.

Kila kitu hakitoshi;

- Ni mtazamo.
- Ni imani.
- Ni mfumo wa maisha.
- Ni u-kawaida ambao wengi wanauishi.

Kwa sehemu kubwa ndio tulivyoshuhudia ndugu zetu, wazazi wetu, marafiki na jamii inayotuzunguka ikiishi hivyo.

Kila kitu hakitoshi,

- Muda-hautoshi kuweza kufanya kile unachotaka kufanya.
- Hela ulizonazo – hazitoshi kuwa mtaji.
- Ujuzi ulionao – hautoshi kuanzisha ulichosema utaanzisha.
- Connection (watu unaofahamiana nao) hawatoshi kukusaidia kuishi ndoto yako kubwa.

Kila kitu hakitoshi.

KWA NINI KILA KITU HAKITOSHI?

“Kinachowatofautisha watu wanaoweza kufanya vitu na wale wanaona kila kitu hakitoshi SIO WINGI/UPUNGUFU WA RASIRIMALI mkononi mwao: kinachowatofautisha ni NINI WANAFIKIRI JUU WA VITU WALIVYONAVYO.”

Dunia imagawanyika katika makundi mawili ya watu,

Makundi haya mawili yametengenezwa na nini watu wanaamini, kuamini kunawapa kufikiri, na kufikiri kunawapa kufanya maamuzi ya kutenda wanavyovitenda.

Kuna watu wanaamini; KILA KITU HAKITOSHI (haiwezekani) na wengine wanaona KILA KITU KINAWEZEKANA.

Kundi la 1: KILA KITU HAKITOSHI (Haiwezekani)

Hili ndilo kundi lenye watu wengi zaidi humu duniani. Kila anayeshindwa kufanya kitu (KUSHINDWA KUISHI NDOTO YAKE) kwa sababu kitu fulani hakipo – anaishi kwenye kundi hili.

Hawa ni watu wanaona HAWAWEZI KUFANYA LOLOTE, hawawezi kubadilisha chochote. Maamuzi kuhusu wao na maisha yao kwa sehemu kubwa yako kutegemeana na nini kinaendelea kutokea.

- Hawana kazi – kwa sababu ajira hakuna.
- Amekosa mtaji – kwa sababu mjomba wake alimuahidi hadi sasa hajampatia.
- Hana furaha – kwa sababu amekosa hiki na kile.
- Hawezi kuanza – kwa sababu bado hajamaliza masomo, bado anaogopa au nyumbani kwao wamepingana na mawazo yake.
- Hajiamini – kwa sababu wengine wengi hawaamini kile anachokiamini yeye.

KILA KITU HAKITOSHI ndio uhalisia wa maisha yaliyopo kwenye jamii nyingi.

Vijana wengi wako radhi kuishi hivi, kuamini hivi, na kuendelea kukubaliana na HAIWEZEKANI (kila kitu hakitoshi) na pengine kuanza kufikiri serikali inapaswa kubeba wajibu kuhusu wao.

Shida kubwa ni kwamba KINACHOKOSEKANA SIO VITU ila UFAHAMU

UNAOWEZA KUONA VITU VIDOGO VINAWEZA KUFANYA VITU VIKUBWA.

**

Mwaka mmoja na zaidi toka nilipomaliza mtihani wangu wa mwisho: BADO NILIENDELEA KUONA HAIWEZEKANI.

Katikati ya fursa zilizonizunguka, Katikati ya watu waliokuwa tayari kunisaidia, Pamoja na kuwa na muda, sehemu nzuri ya kukaa na fedha zilizotosha kuwa mtaji. BADO NILIONA HAIWEZEKANI.

Haikuwa inawezekana – kwa sababu SIO WINGI WA VITU NDIO ULIOKUWA UNAWEZA KUAMUA – ila nini nafikiri; na tatizo kubwa nililokuwa nalo lilikuwa ni “kudhani vitu ndio vinaweza kuleta tofauti”

Msingi wa uzalishaji, ujasiriamali na utajiri uko kwenye namna mtu anavyofikiri. Kama vijana wetu wataendelea kufikiri ni wingi wa vitu ndio unaoleta uwezekano – HAKUNA TUMAINI LA BADILIKO.

Kitabu hiki kwa sehemu kubwa ni kumsaidia mtu – kupiga hatua, kutoka kwenye kufikiri ni vitu ndio sababu na kuanza kuona ni NAMNA ANAVYOFIKIRI NDIO SABABU.

Ukiwa mfuatiliaji mzuri wa historia za biashara, taasisi na kila mtu aliyefanikiwa; utagundua kitu kimoja ambacho wote wamekipitia ni KUANZIA CHINI: kuanzia kwenye “sifuri”. Kuanzia kwenye mazingira ambayo hayakuwa yanaruhusu kuongea ndoto zao kubwa, kuanzia kwenye uhalisia uliokuwa kinyume kabisa na kule walikokuwa wanaelekea.

Suala, SIO WINGI WA VITU: ila NINI KINAWEZA KUFANYIKA NA KIDOGO KILICHOPO?

Bado naikumbuka vizuri sana siku ile, Nilikuwa chumbani kwangu, nikiwa katika meza yangu ya kujisomea/kufanyia kazi.

Sikuwa na furaha wala sikuwa najiamini. Yaani maisha yote yalikuwa yamepoteza ladha, Nilifikia hatua ya kuanza kuona pengine kila ndoto niliyonayo ni mapicha picha tu: haiwezekani na zinanichelewesha.

Ghafla! Wazo likakatiza katika kichwa changu: “VIPI KAMA UKIACHANA NA KILA KITU ULICHOKOSA NA KUANZA KUJIULIZA NINI UNAWEZA KUFANYA KWA VICHACHE HIVI ULIVYONAVYO?”

Huu ndio ilikuwa wa badiliko,

Nikaanza kufikiri…

NINI NAWEZA KUFANYA na “vichache’ hivi MIKONONI MWANGU?

Vitu sio kitu halisi bali nini unaona vitu vinaweza kufanya ndio uhalisia.
Muda, fedha, uhusiano, elimu, uzoefu – vyote sio vitu halisi, kama HAKUNA UNACHOONA UNAWEZA KUFANYA.

Vitu vinaweza kuwa vingi sana, lakina kama hakuna uwezekano unaouna – uwezekana wa kufanya lolote. Vingi havina thamani.

Kinyume chake ni kweli! Hata kama ni kidogo kiasi gani: ukiwa unaona kuna kitu kinawezekana kufanyika – umefanikiwa.

Swali sahihi la kujiuliza ni: NINI NAWEZA KUFANYA NA HIKI NILICHONACHO SASA HIVI?

Kundi la 2: KILA KITU KINAWEZEKANA (Nini naweza kufanya kwa “vichache hivi mkononi mwangu”)
Hili ni Kundi la pili la watu wachache na ndio kundi lenye watu wanaofanikiwa, na wenye matokeo makubwa. Na ndio watu wanaoweza kuleta mabadiliko na kuanzisha vitu mbalimbali (kuziishi ndoto zao).